Kiswahili HIV Budget 10/6/06 10:37 AM Page 2



**Umbo 3: MGAO KWA MAENEO YA VIPAUMBELE KWA 2006/7**




## Mueleko kisera:

Mambo yafuatayo yanajitokeza kutoka kwenye mchanganuo huu na yanahitaji mjadala mpana kwa wadau wote, wakiwemo watengeneza sera, wanaharakati, watu wanaoishi na VVU na jamii kwa ujumla.

- Ukizingatia kuwa fedha zinazotolewa kwa ajili ya VVU na UKIMWI zimepungua (kama sehemu ya bajeti yote ya matumizi ya hiari), je ni halali kusema kuwa sekta hii ni ya kipaumbele kwa serikali na wafadhili?
- Wakati serikali imetangaza kuwa UKIMWI ni janga la kitaifa, je mgao wa pungufu ya 2.5% ya bajeti yote kwenye eneo hili inaonyesha uzingatiwaji wa msimamo huo?
- Pamoja na kuwa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI umetengewa kiwango cha 42% ya bajeti yote ya VVU na UKIMWI, bajeti haionyeshi kwa undani ni aina gani ya shughuli zinaangukia kwenye majukumu ya mpango huu. Ni kwa namna gani hali hii italeta uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha hizo?
- Hatua za uzuiaji wa maambukizi ambazo zinapaswa kuwalinda wale ambao bado hawajaaambukizwa na kuzuia wale ambao tayari wameambukizwa kuendelea kuambukizwa imetengewa 1% ya bajeti yote ya **VVU na UKIMWI**. Je,hii inakidhi mahitaji ya kimkakati ya kuzuia janga hili?
- Ni kiwango gani cha bajeti kitaifikia jamii na walengwa ukilinganisha na kile kinachobaki katika ngazi ya Taifa?
- Je, huduma majumbani inatengewa fedha za kutosha ikizingatiwa nafasi kubwa inayochukua katika kuwahudumia watu wanaoishi na VVU pamoja na magonjwa mengine?

**VVU NA UKIMWI NI JANGA LA KITAIFA.........JE, BAJETI INASEMAJE?**
**na *Kikundi cha Wanaharakati Dhidi ya VVU na UKIMWI. Toleo la Mchanganuo Wa bajeti, Agosti, 2006***

*Muhtasari huu wa bajeti umeandaliwa na kikundi cha wanaharakati dhidi ya VVU na UKIMWI cha baraza la sera la mashirika yasiyo ya kiserikali (Policy Forum). Kikundi hiki kimeundwa na mashirika 15 yasiyokuwa ya kiserikali[ya kitaifa na kimataifa] yanayojihusisha na masuala ya VVU na UKUMWI. Kikundi hiki kina malengo makuu manne ambayo ni kama ifuatavyo:*

1. *Kutoa mrejesho wa matokeo muhimu ya utafiti juu ya sera, matumizi ya umma pamoja na bajeti kama inavyo husiana na upunguzaji wa umaskini na VVU na UKIMWI kwa hadhira kubwa ya mashirika yasiyo ya kiserikali.*
2. *Kujishughulisha kikamilifu kwenye michakato ya sera ya kitaifa inayohusiana na upunguzaji wa umaskini na VVU na UKIMWI,hii ikiwa ni pamoja na uandikaji wa ripoti, kutoa mchanganuo, uteteaj,i utekelezaji na usambazaji wa taarifa.*
3. *Kuwezesha mashirika yasiyo ya kiserikali kufuatilia utekelezaji wa mkakati wa kitaifa dhidi ya VVUna UKIMWI pamoja na MKUKUTA kama unavyohusiana na VVU na UKIMWI*
4. *Kushirikiana na mitandao mingine ya mashirika yasiyo ya kiserikali yanayojihusisha na masuala ya VVU ili kuweza kupata sauti ya pamoja.*

## Kwanini Kuwe na Muhtasari wa Bajeti?

Tangu mwaka 1983,tulipotambua kwa mara ya kwanza kuwepo kwa VVU na UKIMWI nchini kwetu, ugonjwa huu umeeendelea kuenea katika mikoa yote na katika makundi mbalimbali ya kijamii. Katika mwezi Desemba 1999, ugonjwa huu ulitangazwa kuwa janga la kitaifa na serikali ilitambua kuwa muitiko wa sekta nyingi uinahitajika. Kikundi cha wanaharakati dhidi ya VVU na UKIMWI kinatoa muhtasari huu wa mchanganuo wa bajeti ili kuifanya jamii na watoa maamuzi kutafakari kwa makini kama bajeti iliyopo inazingatia VVU na UKIMWI kama jambo la kupewa kipaumbele kadri yasemavyo makundi mbalimbali ya jamii pamoja na mkakati wa kitaifa wa kupambana na UKIMWI.

## Utangulizi

Muhtasari huu umeandaliwa kutokana na bajeti ya mpango wa kati wa matumizi ya serikali kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na TACAIDS pamoja na muhtasari wa bajeti ya afya kwa mwaka 2006/7. Muhtasari huu unalinganisha bajeti ya VVU na UKIMWI kwa mwaka 2005/6 na mwaka 2006/7 kwa kuangalia matumizi ya jumla, matumizi kama sehemu ya bajeti nzima, na mgao wa matumizi kulingana na maeneo ya vipaumbele. Kwa kuzingatia muitikio wa sekta mbalimbali, fedha zilizotengwa kwa ajili ya VVU na UKIMWI zinapatikana katika maeneo mengine zaidi ya TACAIDS na Wizara ya afya na Ustawi wa jamii. Pamoja na hivyo, mgao wa fedha kwenye sekta hizi ni kigezo kizuri kuonyesha msimamo wa serikali katika kupambana na janga hili. Pia, siyo fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya VVU na UKIMWI zinapitishwa kupitia vitabu vya bajeti. Mchanganuo wetu umezingatia mafungu ya fedha yaliyopo kwenye vitabu vya bajeti kwa TACAIDS na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Kiswahili HIV Budget 10/6/06 10:37 AM Page 3






### Mgao wa Bajeti ya VVU na UKIMWI kwa 2005/6 Na 2006/7

**Mhimili namba 1** hapo chini unaonyesha mgao wa fedha kwa VVU na UKIMWI kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na TACAIDS kwa mwaka 2005/6 na 2006/2007. Kwa ujumla, inaonekana kuwa kuna ongezeko la shilingi billioni 9.7 kwa fedha kwa ajili ya VVU na UKIMWI kutoka 2005/6 mpaka 2006/7. Ongezeko hili ni kama 10% ikiwa ni ongezeko la kiasi cha shillingi billioni 7 kwa TACAIDS na billioni 2 kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

| | Mwaka 2005/6 | | Mwaka 2006/7 | |
|---|---|---|---|---|
| | Mgao (Mabillioni ya shilingi) | % Matumizi ya jumla ya hiari ( pasipo vizuizi) | Mgao (mabillioni ya shillingi) | % Matumizi ya jumla ya hiari |
| TACAIDS | 23.6 | 0.70 | 30.4 | 0.67 |
| Wizara ya Afya na ustawi wa Jamii | 66.9 | 1.97 | 69.4 | 1.52 |
| Jumla VVU & UKIMWI | 90.5 | 2.67 | 99.8 | 2.19 |
| Matumizi ya jumla ya Hiari | 3,388.7 | | 4,562.8 | |

Pamoja na ongezeko hilo, ili tuweze kuangalia iwapo kweli VVU na UKIMWI vimepewa kipaumbele kama janga la kitaifa, lazima pia tulinganishe mgao huo na jumla ya matumizi ambayo serikali inatarajia kutumia (hii ina maana ya fedha inayobaki katika matumizi yote ukiondoa fedha za matumizi ya ikulu na kulipia madeni ya nchi). Tukifanya ulinganifu huu, tunaona kuwa mgao wa fedha kwa ajili ya VVU na UKIMWI

VVU NA UKIMWI NI JANGA LA KITAIFA.........JE, BAJETI INASEMAJE?
na *Kikundi cha Wanaharakati Dhidi ya VVU na UKIMWI. Toleo la Mchanganuo Wa bajeti, Agosti, 2006*

unapungua kutoka 2.67% kwa 2005/6 hadi 2.19% kwa 2006/7. Nyongeza hii inaonekana vyema kwenye jedwali na.1 hapa chini.

### Jedwali namba 1. Mgao wa bajeti ya VVU na UKIMWI 2005/6 na 2006/7

Kupungua kwa mgao wa **VVU na UKIMWI** kutoka kwa mapato ya jumla ya hiari kunaonekana vile vile kwenye **mhimili na.2** hapo chini. Kwa ujumla, ukizingatia takwimu zilizo wazi kwa umma, ndani ya bajeti,kuna mapungufu ya matumizi yaliyotengwa kwa VVU na UKIMWI kwa 0.48% kutoka 2005/6 mpaka 2006/7; ambayo ni kama shillingi billioni 21.9. Kwa ujumla,serikali inapanga kutumia 2.2% ya fedha zote zilizopo kwa mwaka 2006/7, kwa ajili ya VVU & UKIMWI. Hii inaleta maswali iwapo kweli VVU na UKIMWI vimepewa kipaumbele kama janga la Taifa.




### Mgao wa Bajeti ya VVU & UKIMWI Kwenye Maeneo ya Vipaumbele kwa 2006/7

Mkakati wa Taifa wa VVU na UKIMWI unaohusisha sekta mbalimbali umeorodhesha maeneo ya vipaumbele katika kudhibiti VVU na UKIMWI. Maeneo haya ni uzuiaji wa maambukizi, utunzaji na uegemezi, upunguzaji wa makali ya athari na mambo mtambuka. Tunahitaji kuchunguza mgao kwenye maeneo haya ya kipaumbele na kujadili iwapo mgao huo ni wa kimkakati katika kukabiliana na janga hili.

**Umbo namba 3** hapo chini linaonyesha kwamba 26% ya matumizi ya TACAIDS hayakubainishwa kwenye maeneo ya vipaumbele. Pili, inaonyesha vilevile kuwa mafungu ya Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP), chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, pamoja na ukubwa wake (42%) hayaonyeshwi kwa undani jinsi yatakavyotumika. Takwimu zilizopo (Tanzania HIV/AIDS Indicator Survey 2003-2004) zinaonyesha kuwa 93% ya watanzania watu wazima hawajaaambukizwa .Pamoja na hivyo, ni 1% tu ya bajeti imeelekezwa kwenye uzuiaji. Tatu uchambuzi wa bajeti ya Wiazara ya Afya na Ustawi wa jamii kwa mwaka 2006/7 unaonyesha ni shilingi milioni 92.7 tu kati ya bilioni 26.2 (0.35%) zilizotengwa kwa ajili ya huduma majumbani.